



MATUMIZI YA DAWA ZA KIASILI No. TNP1

Pilipili, *Capiscum frutescens*

Pilipili kali ilitokea Amerika ya Kusini na kusambaa kote duniani katika nchi za hari na zile za ukame. Viungo vya kuuu na kuzuia wadudu vimekolea katika matunda yaliyoiva na mbegu zake. Pilipili husababisha mwasho mkali na huzuia aina mbalimbali ya wadudu.

Fahamu Tahadhari yapaswa kuchukuliwa unapotumia pilipili kali kwa sababu yaweza kudhuru macho na ngozi.

Matayarisho

- **Dawa ya kunyunyuzia ya pilipili 1**

Ponda ponda vikombe 4 vya pilipili au vikombe 5 vya mbegu yake. Weka kwenye sufuria iliyo na lita 3 za maji kisha kuchemsha kwa dakika 15-20. Toa kwenye moto halafu ongeza lita 3 za maji. Chuja kwa kutumia kitambaa na hifadhi maji uliyochuja. Ongeza sabuni ili mchanganyiko huo unyunyiziwe kwenye wadudu na majani. Tumia sabuni yenye *Potash* kama ile ya kuosha vyombo wala usitumie sabuni zenye *Caustic Soda* (kwani hudhuru mimea).

Jinsi ya Kutumia: Nyunyiza kwa kutumia majani au nyasi iliyofungwa kwa pamoja. Nyunyiza mara moja kwa wiki lwapo hakuna mvua au mara mbili au tatu kama kuna nyesha.

lwapo mchanganyiko hautayeyushwa, waweza kudhuru mimea. Hivyo basi tahadhari yapaswa kuchukuliwa.

- **Dawa ya kunyunyuzia ya pilipili 2**

Kata gramu 500 za pilipili iliyoiva na uweke ndani ya ndoo iliyojaa maji. Wacha ioze kwa siku 4 au 5. Chuja mchanganyiko na uhifadhi maji uliyochuja. Kisha changanya gramu 30 za sabuni na maji uliyochuja. Nyunyizia ukitumia kifaa cha kunyunyiza au majani uliyofunga pamoja. Tumia sabuni iliyo na *Potash* kama ile ya kuosha vyombo wala sio yenye *Caustic Soda* ambayo hudhuru mimea.

Jinsi ya kutumia: (Utaratibu ni kama wa 1)

- **Dawa ya kunyunyuzia ya pilipili na kitunguu Saumu**

Ponda ponda kitunguu saumu kisha uongeze kikombe kimoja cha maji. Ongeza kijiko kikubwa cha uvugu wa pilipili. Koroga kwenye lita 2 za maji moto, halafu uache mchanganyiko upoe. Chuja kwa kutumia kitambaa laini kisha uongeze maji. Ongeza sabuni kisha kuvuruga.

Jinsi ya kutumia: Tumia kwa kuzuia aina mbalimbali ya wadudu.

- **Dawa ya kunyunyizia ya Pilipili kali, Tururu na Vitunguu**

Chukua kiasi kidogo cha pilipili (4) kisha changanya na Tururu pamoja na vitunguu maji. Loweka mchanganyiko kwa siku moja kwenye maji ya sabuni. Tumia sabuni aina ya *Potash*. Chuja kwa kutumia kichujio kisha uongeze lita 2 za maji.

Jinsi ya kutumia: Tumia kwa kuzuia buibui.

- **Unga wa pilipili**

Pondaponda pilipili kiasi utakachoweza.

Namna ya Kutumia: Nyunyiza unga wa pilipili karibu na shina la mimea ili kufukuza wadudu kama mchwa na wadudu wengine wa ardhini.

Matumizi Mengine

Kupanda kwa pamoja: Pilipili zaweza kupandwa pamoja na mimea ya chakula kuzuia wadudu, viyoga, na vijidudu wengine.

Maelezo haya yanaweza kunakiliwa bure kwa njia yoyote pasipo malipo.

Tafsiri na;

Seth Manera, Vihiga, Kenya. May 2004 Email: sethmanera@yahoo.com

Swahili Series Editor: **Patrick Bunyali Kamoyani**

Email: pbkamoyani@excite.com or pbkamoyani@lycos.co.uk

Produced by The Tropical Advisory Service, June 2000

This update: Jan 2005

HDRA - the organic organization, Ryton Organic Gardens Coventry CV8 3LG UK
Tel +44 (0)24 7630 3517 Fax +44(0)24 76623 9229 Email: ove-enquiry@hdra.org.uk

Website: <http://www.hdra.org.uk>

Madhumuni ya shirika la HDRA ni kufanya utafiti, kutoa na kueneza habari kuhusu Kilimo Hai, Ukulima na chakula katika Uingereza (UK) na Dunia nzima. Mwongo mmoja uliopita, shirika hili limekuwa likisaidia katika kubuni njia za kuboresha na kutafiti aina ya ukulima hasa Kilimo Hai katika nchi za hari (Tropics). Vilevile kutoa maelezo na majarida kuhusu Kilimo Hai na pia kutoa mbegu na maelezo ya upanzi. Shukrani nyingi ni kwa Charlton Community Development Trust kwa mchango wao kuona makala haya yamechapishwa.